mmojawapo wakwisusiriwa na Roho, ipate murimbisiwe. 12 Caniri kwamba ndi-ci:
tirimbisane myoyo nkati ya kwamini kwetu kumoja, kwenu umwe na kwangu omi.
13 Wanduzangu, vinajibu mwijiwe kuwa nipanga mara nyingi zawenye kuja kukuwo-
nani, fala mpaka sambi-pa sinapata nafasi. Vinajibu niwatenze wanu wamojawapo
wamwamini na wanfulate Insa, kati yenu umwe na novyo kati ya wanu wengine
Sawari-Mayahudi. 14 Kusema kweli, vinilazimu kuwasaidiya wanu wa tabiya yetu na
wanu wa tabiya nyengine, wanu wakusilimuka na wanu sawasilimuke. 15 Ntamana,
niwa radi kuja kwenu mwikala Roma-mwe kukwerezani Habari Ngema.
16 Kusema kweli, siwona haya kwa eyi Habari Ngema-yi konta ndi uwezo wa
Mwenyezimungu kuwavusha piya wenye kumwamini, mwanzo wa Yahudi mpaka
Saari-Yahudi. 17 Kamana ukamilifu wa Mwenyezimungu* ufafanuriwa nkati ya Habari

* **1:17** "Ukamilifu wa Mwenyezimungu" mana ake, namuna iye vyawatenza wanu kupatana naye.

Ngema, namuna za kwamini mwanzo mpaka mwinsho. Kamba vyavyandikiwe:
“Kamilifu áinshi julu ya kwamini.”

### *Wabaya walamuriwa hukumu*

18 Ifafanuriwa nyongo ya Mwenyezimungu binguni julu ya piya kutowa kuwepo
ka dini na kukosa ukamilifu ka wanu, julu ya kutowa ukamilifu-ko, ndi kuwatenza
wanu kufuja ukweli. 19 Kamana ukweli kuhusu Mwenyezimungu ufafanuriwa kati
yawo, kwa kuwa Mwenyezimungu kawafafanurira. 20 Tangu kumbiwa ulumwengu,
namuna zake saziwoneka, kwa nfano uwezo wake sauna mwinsho na unlungu wake,
vyeleweka na vijiwikana sana-sana julu ya vinu vyaatenda Mwenyezimungu. Basi
ewo awana shariya yakolota. 21 Kamana ingawa wamwijiwa Mwenyezimungu, fala
awantukuze kamba Nlungu wawo wala awanshukurire. Kwasa javyo, wanza kufikiri
mawazo saana mana, na myoyo yawo iwazizima, ikingíziwa nkisi. 22 Waritula kuwa
wejiwifu kumbe mazozo. 23 Wasa kumwambudu Mwenyezimungu saabadilika, wapin-
dula wambudu maswanamu a wanu wakubadilika, a nyuni, a wadudu pamoja na a
manyoka.

24 Ntamana, Mwenyezimungu kawasa watende viwájibu myoyo yawo, vitendo vya
ucafu, watebeni miri yawo wanyewe. 25 Iye awatenda javyo konta wapindula ukweli
wa Mwenyezimungu wafulata ulongo. Novyo, wamwabudu na wantumika kiyumbe,
wasa kumwambudu Mwenyé kumba wawenye. Iye ájuzi asifiwe milele! Aamina.

26 Ntamana, Mwenyezimungu kâwasa watende vitendo vyawo vyakuwajibu
vyakuwatenza aibu. Anta na wanawaka wapindula namuna yawajuzi kuloriwa na
walume wawo, wanza kulolana wanawaka watupu. 27 Namuna mmoja noyo, walume
wasa kuwalola sana waka wawo, yanza kuwalunguza myoyo kwajibiwa pakulu na
walume wenziwawo. Walume watupu watenda vitendo vya aibu, ntamana nkati yawo
hukumu iwajuzire kwa makosa awo waritabisha wanyewe.

28 Kwa kuwa awolote kumwijiwa Mwenyezimungu, iye kawasa na ankili zawo za
ubaya, watende vitendo sawajuzi kutenda. 29 Myoyo yawo ijala udainfu wa kila
namuna, kusiyanisa masemo, ulwaziwa moyo, na ubaya. Kusema kweli, uwejala
nfululu wiyana, ukakatima, wivu, ulongo, na uzuda. Walawirira kuwa wasemisemi,
30 wanu wakuwasowerera caputu wenziwawo, wamwina Mwenyezimungu, majauri,
wakuritenza, wakuridãi, wakubuni vinu vibaya, na wakubishana na wawa zawo.
31 Ewo awana ankili, awana kwamini, awampenda munu, na awana utungu. 32 Ewo
wakwijiwa sana-sana shariya za Mwenyezimungu, kuwa wanu watenda novi vi-
tendo-vi wajuzi waulaiwe. Evi vitendo-vi awatenda tu basi fala wawetikizira wengine
watenda.

# 2

### *Walamuriwa hukumu wenye kuwalamula wenziwawo*

1 Ntamana auswamiiwa, uwe mwenyé kulaumu. Kamana unlaumu munu
mwengine, kumbe kwankurilaumu mwanyewe. Konta uwe kwankutenda vitendo
vimoja novyo vyaulaumu-vyo. 2 Tukwijiwa kuwa Mwenyezimungu, paabishana
na wanu watenda vinu-vi, hukumu yake ifulata shariya. 3 Tunza javi, uwe munu
mmojawapo, uwalaumu watenda vitendo nnowe ukitenda novyo, udaniza kuwa
utakunyema hukumu ya Mwenyezimungu? 4 Au kwankukejeli utajiri wa wema wa
Mwenyezimungu, na kuvumirira kwake, pamoja na imani yake? Awijiwa kuwa wema
wa Mwenyezimungu ukulongoza upate kutubiya? 5 Fala uwe, kwa sababu ya ugumu
wa moyo wako pamoja na ubishi, kwankurongeza nyongo ikupate uwe mwanyewe
suku yakwisuka nyongo, na suku yakolotiwa hukumu ya haki ya Mwenyezimungu.

6 Iye mwenyé kunludisira kila mmoja kwa kitendo caatendire: 7 upande mmoja,
wasakúla utukufu, inshima, na uzima julu ya kutenda vinu vyema-vyema kwa kuvu-
mirira, Mwenyezimungu awapa mainsha a milele. 8 Upande mwengine wafitíni na
awafulata ukweli, wafuláta kukosa haki, Mwenyezimungu akimiyana nawo na nyongo
pakulu. 9 Zije tabu na shida kwa kila mwanadamu aténda ubaya, mwanzo wa Mayahudi
na novyo Sawari-Mayahudi, 10 ila uje utukufu, inshima, pamoja na usalama kwa
kila mwanadamu aténda meema, mwanzo wa Mayahudi na novyo Sawari-Mayahudi.
11 Kamana akupo kusiyana ka wanu mbere ya Mwenyezimungu. 12 Wakorire dambi
sawana shariya, newo novyo sawana mpaka wa shariya wapoteya. Ila wakorire dambi
wari na shariya, shariya noyo iwahukumu.

*Walamuriwa hukumu Mayahudi*

13 Kamana sikuwa wasikíra shariya kuwa ndi makamilifu mbere ya Mwenyezimungu
ila ware waja kwakikishiwa ndi waténda vyaisaka shariya. 14 Kamana wanu Sawari-
Mayahudi sawana shariya, wakitenda vyaisaka shariya kwa kipongorero, ingawa
awana shariya, wakolota kuwa wakwijiwa wanyewe shariya ya cema na kibaya. 15 Ewo
wakolota kuwa shuruti ya shariya yandikiwa mmyoyo yawo. Fahamu zawo pamoja
na ankili zawo zilavya ushahidi. Wakati mwengine ziwalaumu, wakati mwengine
ziwengirira, suku ya Kiyama. 16 Suku-yo, kwa kufulata utuba wangu, Mwenyezimungu
julu ya Almasihi Insa alamula siiri za wanu.

17 Ona, uwe uritula kuwa Yahudi, utejemera shariya, na uridãi kuwa munu maalumu
mbere ya Mwenyezimungu. 18 Ukwamba kuwa ukwijiwa vyaasaka iye, na vikwajibu
vinu bora vyaufundiwe kati ya shariya. 19 Ukuwa na uhakika kuwa uwakorera
nkongojo vipofu, na kuwa nuru ka wanu wenenda pakisi, 20 uwalongoza wenye
kutikina, kuwa mwanlimu wa wanemba, na kuwa nazo namuna za wijiwifu na ukweli
nkati ya shariya. 21 Uwe uwafunda wanu wengine, kutowa kurifunda mwanyewe
sababuni? Uwe ukwereza kuwa munu aajuzi kwiwa, uwe wiwaja? 22 Ukwamba munu
asizinge, sambi, uwe uzingaja? Ukwamba kuwa ayukwajibu milungu ya ulongo, sambi,
upitaja ukiiwa mmanyumba a dini? 23 Uwe úridãi kwijiwa shariya, fala aufulata noyo
shariya-yo, kwankunkejeli Mwenyezimungu, sinovyo? 24 Kamana Mandiko akwamba
javi:

“Zina ra Mwenyezimungu riwankukejeliwa na wanu Sawari-Mayahudi kwa sababu
zenu umwe.”

25 Kusema kweli, itani yanawo faida ukitimiza shariya. Fala ikiwa kuwa nvunji wa
shariya, ukuwa kamba sawingire itani. 26 Ikiwa wanu sawengire itani ndi wafuláta
shariya, awaturiwa nowo kamba wanu wengire itani? 27 Ntamana wanu sawengire
itani watimíza shariya, ewo wakulaumu kwa kuwa kwanawo shariya yakwandikiwa
yawenye na kwingira itani, fala aufulata shariya. 28 Kamana iye siyo Yahudi wa
vitendo vya panja tu basi. Itani sikinu, ila kitendo ca panja ca mmwiri tu basi.
29 Fala iye Yahudi* nkati ya roho yake, na itani ndi yengiziwe mmoyo julu ya Roho wa
Mwenyezimungu, siyo julu ya shariya yakwandikiwa. Iye swifa zake sizo za wanadamu
ila za Mwenyezimungu.

# 3

1 Epa, faida yakuwa Yahudi ndi yepi? Au nkati ya itani, cipatikana kinani? 2 Aye,
ziwapo faida nyingi. Faida ya kwanza ndi kuwa Mayahudi wagabiziwa usemi wa
Mwenyezimungu mwanyewe. 3 Iwaja? Mayahudi wamojawapo wakitowa kwamini,
kutowa kauli kwawo, Mwenyezimungu afuja kauli yake? 4 Isiwe javyo, ila ingawa kila

* **2:29** “Yahudi” epa mana ake “swifa”.

mwanadamu nlongo, fala Mwenyezimungu ndi mwenyé ukweli. Kamana mMandiko*
vyandikiwa javi:

"Wakikishiwe nkati ya usemi wako,
ushinde pauja kulamuriwa."

5 Fala ikiwa kutowa kukamilika kwetu kukolota ukamilifu wa Mwenyezimungu,
tambani tena? Tikwamba Mwenyezimungu sikamilifu paatihukumu na nyongo yake?
(Nisowera kamba vyawasowera wanadamu.) 6 Kusema kweli, sivyo! Ikiwa javyo,
Mwenyezimungu ulumwengu-wu alamulaja? 7 Fala ikiwa ulongo wangu ukolota
pakulu ukweli wake ipate iye atukuziwe pakulu, nihukumiriwani kamba mmadambi?
8 Mbana atamba (kamba wanu wengine vyawabuni kuwa tikwamba): "Titende vitendo
vibaya ipate vije vitendo vyema, sinovyo?" Kuhukumiwa kwawo ka haki.

### *Walamuriwa hukumu wanu piya*

9 Kinani tena? Itakuwa ofwe Mayahudi tiwa bora pakulu koliko wengine? Anta!
Tibainisha futi kuwa wanu piya, Mayahudi pamoja na Sawari-Mayahudi, wamilikiwa
na dambi. 10 Mandiko Matakatifu† akwamba:

"Aapo munu kamilifu, anta mmoja.
11 Aapo anta munu mmoja wakwerereriwa sana.
Aapo munu antaja Mwenyezimungu.
12 Piya wanu wanloza minyongo,
waridanganya awafãi kinu.
Aapo atenda meema, aapo anta mmoja.
13 Paulo pawo pawa kamba kaburi ra kuwa wanzu.‡
Kwa malulimi awo walongopa.
Mivumbu yawo ílawa sumu ya nyoka wakofya.§
14 Viwejala pakanywa pawo lana na usowezi wa kuwawa.*
15 Maulu awo akwenenda upesi kusuja damu.†
16 Menenzi awo auwaribifu na ausikini.
17 Awejiwa njira ya usalama.‡
18 Mmaso mwawo awamopa Mwenyezimungu anta aba.§"

19 Sambi, tukwijiwa kuwa piya vyaisema shariya wakwambiriwa ware wenendera
shariya ipate kanywa zawo zinyamare, na piya wanu mulumwengu-mu wajuzi kunjibu
Mwenyezimungu. 20 Kamana kwa vitendo vya shariya aapo munu anta mmoja aja
kwakikishiwa mbere ya Mwenyezimungu. Kamana shariya ndi intenza munu kwijiwa
kuwa kanawo madambi.

### *Almasihi atwala hukumu zetu*

21 Fala sambi, ukamilifu wa Mwenyezimungu* ubainisha namuna nyengine sairi
ya kufulata shariya (ingawa shariya pamoja na mandiko a minabii vilavya ushahidi
kuhusu ukamilifu-wo). 22 Ukamilifu wa Mwenyezimungu uwa julu ya kauli ya Insa
Almasihi, kwa piya wenye kumwamini. Kati ya wanu akupo kusiyana, 23 konta wanu
piya wakola dambi na uwapunguka utukufu wa Mwenyezimungu. 24 Wanu piya
wakikishiwa kwa rehema yake bila maripo, julu ya komboriwa na Insa Almasihi.
25 Mwenyezimungu wantondore kuwa awe kafara yakupatanisa julu ya damu yake ka
ware wenye kuntumaini, iwa ipate olote ukamilifu wake. Mida, kwa sababu ya imani

---

* **3:4** Ona Zaburi 51:4. † **3:10** Ona Zaburi 14:1-3. ‡ **3:13** Ona Zaburi 5:9. § **3:13** Ona Zaburi 140:3. * **3:14** Ona Zaburi 10:7. † **3:15** Ona Izaya 59:7. ‡ **3:17** Ona Izaya 59:8. § **3:18** Ona Zaburi 36:1. * **3:21** Ukamilifu wa Mwenyezimungu ndi namuna yake yakulamula haki.

yake, iye akitowa kuhukumu madambi a munu akorire. 26 Epa sambi, Mwenyezimungu
kantondola Insa kuwa kafara yakupatanisa ipate wakati-wu olote ukamilifu wake,
kuwa iye ndi mwenyé shariya na wakumwakikisha ire antumaini Insa.
27 Kwa javyo, tiridãi sababuni? Kuridãi akupo. Kwa shariyani? Kwa shariya ya vi-
tendo? Anta, kwa sababu ya kwamini. 28 Konta tijiwa kuwa munu ápatana na Mwenyez-
imungu julu ya kumwamini Insa, siyo julu ya kutimiza shariya. 29 Mwenyezimungu
Nlungu wa Mayahudi tu basi? Níkamba Nlungu wa wanu Sawari-Mayahudi novyo? Ndi
kweli, wawo na Sawari-Mayahudi newo novyo! 30 Kamana Nlungu ndi mmoja, na iye
antenza munu kupatana naye julu ya kumwamini, awe Yahudi au Saari-Yahudi. 31 Kwa
javyo tifuja shariya kwa sababu ya kwamini? Kusema kweli, anta! Ila na shariya, neyo
tukwakikisha.

# 4

*Nfano wa kwamini wa Iburahima*

1 Kwa javyo, kuhusu Iburahima, wawa wa mataifa etu kibinadamu, iye kapata
kinani? 2 Kamana ikiwa kakikishiwa julu ya vitendo vyake, kanawo haki ya kuridãi,
ila aawa nawo haki-yo mbere ya Mwenyezimungu! 3 Kamana Mandiko akwamba javi:

“Iburahima kamwamini Mwenyezimungu,
ntamana Mwenyezimungu kamwisabu kuwa kamilifu.”

4 Sambi, nshahara waapokera nkolakazi siyo zawadi ila deni. 5 Na munu saatumaini
kazi yaatenda ila antumaini ire amwakikisha mbaya, kwamini kwake ndi kuntenza
iye awe kamilifu. 6 Kwa namuna moja noyo, Daudi kuhusu heri ya munu wakuwa
Mwenyezimungu ankubali kuwa kamilifu bila kwisabu vitendo vyaatendire,* kaamba:

7 “Heri wenye kuswamiiwa makosa awo,
ware wafutiwe madambi awo!
8 Aye, heri munu wakuwa Mwenye aaisabu dambi zake!”

9 Sambi, noyi heri-yi itakuwa ya wenye kwingira itani tu basi, au na ya wanu
sawengire newo novyo? Kamana tikwamba kuwa Iburahima kesabiwa kuwa kamilifu
kwa sababu ya kwamini kwake. 10 Kesabiwa rini? Iwa esire kutaiwa itani, au
saanamba? Iwa saanamba, ila saanataiwa itani! 11 Kusema kweli, iye kapokerera
alama ya itani, iwe kipaji cakuwa mwenyé haki kwa sababu ya kwamini kwake, na evyo
vikuna saanataiwa itani. Vikuna javyo, ipate awe wawa wa wanu piya wamwamini
Mwenyezimungu sawengire itani, na ware wesabiwe kuwa makamilifu. 12 Na iye
ndi wawa wa ware wengire itani, fala siwengire itani tu basi ila newo novyo wari
kulondoza kwamini ka babu yetu Iburahima kábula saanataiwa itani.
13 Kamana aiwere kwa kufulata shariya kuwa ndi citenzire Iburahima pamoja na
ujukulu wake kupokerera tamaa ya kuwa akúja kuriti ulumwengu-wu, ila kwa sababu
ákiwa mwenyé haki julu ya kwamini kwake. 14 Kwa kuwa, ikiwa wafulati shariya ndi
wariti, basi kwamini akufãi na tamaa ifujika. 15 Kamana shariya ikuja na nyongo, fala
mahala saipo shariya, kukosa akupo.
16 Ndi ntamana, tamaa ikuja julu ya kwamini ipate iwe julu ya rehema, na kuhusu
tamaa-yo, piya ujukulu wa Iburahima wawe na uhakika. Siware wafulata shariya basi,
fala na wari na kwamini ka Iburahima, wawa yetu piya-fwe. 17 Kamba vyavyandikiwe:
“Omi nukutula kuwa wawa wa kabila nyingi.”
Iburahima kantumaini Mwenyezimungu, ire awápa mainsha wafwi, na mwenyé
kumba savikiwepo. 18 Ingawa upande wa kibinadamu aikiwepo tamaa, novyo-sivyo

* **4:6** Ona Zaburi 32:1-2.

katumaini na tamaa kuwa álawirira kuwa wawa wa kabila nyingi zawenye, kamba
vyaisemiwe†: "Ujukulu wako ukuja kuwa mwingi." 19 Iburahima aasokeziwe nkati
ya kwamini kwake, ingawa akirinang'aniza mwiri wake wîsa (kwa kuwa hirimu yake
íkiwa kiyasi ca myaka miya), na tumbo ra Sara rîfunga. 20 Novyo-sivyo, iye aasire niya
ya kutumaini tamaa ya Mwenyezimungu ila karimbisiwa na kwamini kwake kuno
akinsifu Mwenyezimungu, 21 konta ákiwa na hakika piya kuwa Mwenyezimungu tamaa
yaalavire, ákiwa nawo uwezo wakutimiza novyo. 22 Ntamana, Iburahima "kesabiwa
kuwa kamilifu". 23 Usemi ukwamba "kesabiwa kuwa kamilifu", aamwamba iye tu basi,
24 ila wandikiwa novyo kwa faida yetu ofwe, tija kwisabiwa kuwa wenye ukamilifu
kamana tintumaini ire anfufure Insa ka wafwi, Mwenye wetu. 25 Insa-yu aperekiwe
kufwa kwa sababu ya madambi etu, na afufuriwe ipate takikishiwe.

# 5

*Salama julu ya kuntumaini Mwenyezimungu*

1 Kwa kuwa takikishiwa julu ya kwamini kwetu, tanawo salama na Mwenyezimungu
julu ya Mwenye wetu, Insa Almasihi. 2 Julu ya kuntumaini Insa, tanawo uwezo
wakupata rehema yatiri nawo-yi. Kusema kweli, tifurahi kwa kuwa tirindira kuwona
utukufu wa Mwenyezimungu.

3 Visitoshe, tifurahi novyo pazitipata tabu, konta tukwijiwa kuwa tabu zitifunda
kuhitamili. 4 Ikisa tena, kuhitamili kutitaya namuna yakusakikana, na namuna
yakusakikana ititaya tamaa. 5 Na eyi tamaa-yi aititenza aibu, konta pendo ra Mwenyez-
imungu rijala mmyoyo mwetu julu ya Roho Takatifu watipewe ofwe.

6 Kamana ingawa tiveya, paufikire wakati wake, Almasihi kafwa kwa ajili ya
makafiri. 7 Kusema kweli, munu kufwa kwa ajili ya mwenyé ukamilifu, virigariga
pakulu. Dalili, munu ákidiri kufwa kwa ajili ya ntenda-mema. 8 Fala Mwenyezimungu
kolota pendo rake kwetu ofwe, kamana Almasihi kafwa kwa ajili yetu ofwe patíkiwa
wamádambi. 9 Ntamana, kwa kuwa takikishiwa na Mwenyezimungu julu ya damu
ya Almasihi, kuzidi pakulu iye akuja kutivusha nkati ya nyongo ya Mwenyezimungu.
10 Kamana, kwa kuwa tipatanisiwa naye julu ya kifo ca Almasihi patikiwa maaduwi
wake, vizidi futi patipatanisiwe-pa, tikuja kuvushiwa julu ya mainsha ake. 11 Visitoshe,
tifurahi novyo ka Mwenyezimungu julu ya Insa Almasihi, Mwenye wetu, konta julu
yake, tipatanisiwa.

*Adamu na Almasihi*

12 Kwa javyo, julu ya munu mmoja ingira dambi mulumwengu-mu, na kwa javyo
cingira kifo novyo. Ikisa kifo ciwapata wanu piya, konta piya wakola dambi. 13 Kusema
kweli, sainamba kuwepo shariya, dambi ikiwapo mulumwengu-mu. Fala, kwa kuwa
aiwerepo shariya, dambi-yo aikiwalangiwa. 14 Novyo-sivyo, kifo cîtawala wanu piya
tangu wakati wa Adamu mpaka wakati wa Musa, anta na ware sawakorire dambi
kamba vyaatupire kauli Adamu. Adamu nfano wa namuna mmojawapo wa munu
akirindiriwa kuja*.

15 Fala kitendo ca neema ca Insa aciri kamba ukosa wa Adamu. Kamana kwa kukosa
munu mmoja† wafwa wanu wengi. Fala kwa rehema ya Mwenyezimungu na ya
munu mmoja Insa Almasihi yolotiwe julu ya meema yake, wengezeka wanu wengi
wakujanliiwa. 16 Novyo, kuwapo kusiyana kuwonekana nkati ya neema na dambi ya
munu mmoja. Konta kulaumiwa kufulata ukosa mmoja ujire na hukumu, fala neema
yesusiriwe munu ifuláta makosa mengi ajire na uhakika. 17 Kamana, ikiwa kukosa
ka munu mmoja, kifo citawala kwa sababu ya noyo munu-yo, kuzidi pakulu ware

† **4:18** Ona Mwanzo 15:5. * **5:14** "Munu akirindiriwa kuja" ndi Almasihi. † **5:15** "Munu mmoja" ndi Adamu.

wapokerere rehema pakulu-pakulu na neema ya uhakika, ewo wakuja kutawala nkati
ya mainsha julu ya munu mmoja, noyo Insa Almasihi-yo.
18 Sambi, kamba ukosa wa munu mmoja vyaujire na hukumu ka wanu piya, ndi
sawa-sawa novyo kitendo kimoja ca kukamilika cikuja na uhakika pamoja na mainsha
ka wanu piya. 19 Kamana, kamba ubishi wa munu mmoja vyawaturiwe wengi kuwa
wenye ukosa, ndi sawa-sawa novyo kwa kusikiriza ka munu mmoja, wengi wakuja
kuturiwa kuwa wenye ukamilifu. 20 Shariya ija ipate yolote sana-sana ukosa wa kutupa
shariya. Fala paizidire dambi, izidi kwijala rehema, 21 ipate, kamba vyaitaware dambi
nkati ya kifo, na rehema novyo itaware, itipe ukamilifu mbere ya Mwenyezimungu,
tipate mainsha a milele julu ya Insa Almasihi, Mwenye wetu.

# 6

*Mwinsho wa uwezo wa dambi*

1 Sambi, tambe mwaja? Tibaki tikiinshi nkati ya dambi, ipate rehema yongezeke?
2 Anta! Ofwe tifwire dambi, tizidija kuinshi na dambi tena? 3 Au mutikina kuwa piya-
fwe toziwa tilungane na Insa Almasihi, toziwa tilungane novyo na kifo cake? 4 Kamana
tizikiwa pamoja naye julu ya kutoza nkifo cake ipate, kamba vyafufuriwe Almasihi
nkifo julu ya utukufu wa Baba, na ofwe novyo tiinshi kwa namuna nyipya.
5 Konta ikiwa tilungana naye nkati ya kifo cake, ndi sawa-sawa novyo nkati ya
kufufuriwa kwake, nofwe tifufuriwa. 6 Tijiwe javi, kuwa umunu wetu watíkiwa mida
ugomezeriwa pansalaba pamoja neye ipate ufujike mwiri wetu wa dambi, tisiwe tena
watwana wa dambi. 7 Kamana mmojawapo afwire onse namuna-yo, komboriwa nkati
ya uwezo wa dambi. 8 Na ikiwa tifwa na Almasihi, tukwamini kuwa novyo tiinshi naye.
9 Tukwijiwa kuwa Almasihi kafufuriwa nkifo, ntamana aafwa tena, kifo acinkidiri tena.
10 Paafwire, kafwa kwa sababu ya dambi, ntamana uwezo wa dambi ushindiwa kwa
milele. Na sambi, nkati ya uhai wake, kankuinshi vyavimwajibu Mwenyezimungu.
11 Kwa javyo, nnomwe novyo ritureni wanyewe kamba mufwire, uwezo wa dambi
ushindiwe, fala kwa kuwa mulungana na Almasihi Insa, mwankuinshi vyavimwajibu
Mwenyezimungu.
12 Kwa javyo, musase dambi kutawala mwiri wenu kusikiriza wájibu wenu wa vitendo
vibaya. 13 Musipereke vifingo vya mwiri wenu kudambi, kutenda vinu savina shariya.
Ila, riperekeni umwe ka Mwenyezimungu kamba wanu wakulawa nkifo ipate muinshi
ka ukweli. Riperekeni vifingo vya mwiri wenu kuwa combo ca kutenda shariya ka
Mwenyezimungu. 14 Kamana dambi aikukidirini, konta amutawariwa na shariya,
muinshi julu ya rehema ya Mwenyezimungu.

*Uhuru wakuntumika Mwenyezimungu*

15 Mana ake kinani? Tikore dambi kwa kuwa atiri sini yakumilikiwa na shariya ila
timilikiwa na rehema? Anta! 16 Amwijiwa kuwa mukiripereka ka munu kuntumika na
mukinsikiriza kamba watwana, muwa watwana wamuntumika mukinsikiriza noyo?
Anta iwe musikiriza dambi mwinsho íja na kifo, anta iwe munsikiriza Mwenyez-
imungu, mwinsho ája na uhakika. 17 Fala shukuruni ka Mwenyezimungu! Ingawa
mida múkiwa watwana wa dambi, fala sambi musikiriza kwa myoyo yenu ngano
zamugabiziwe. 18 Basi, momboriwa mmakono mwa dambi, mulawirira kuwa watwana
wa njira ya uhakika. 19 Omi nisowera kwa kutumira nfano wa kibinadamu konta ankili
zenu aba. Umwe mida mupereka vifingo vyenu kuwa watwana wa ucafu na udainfu
pakulu. Epa sambi, riperekeni vifingo vyenu viwe watwana wa njira ya haki ipate
muwe watakatifu.
20 Pamúkiwa watwana wa dambi, múkiwa na uhuru amukifulata njira ya haki.
21 Faidani yamupatire nowo wakati-wo? Mukitenda vitendo vyamuriwonera haya

kutenda sambi-pa, na mwinsho yawo novyo vitendo-vyo ndi kifo! [22] Fala sambi, kwa
kuwa momboriwa nkati ya uwezo wa dambi, mulawirira kuwa watwana wa Mwenyez-
imungu, mupata faida yenu ya kuwa watakatifu, na mwinsho ndi mainsha a milele.
[23] Konta nshahara wa dambi ndi kifo, fala kitendo ca neema ya Mwenyezimungu ndi
mainsha a milele julu ya Almasihi Insa, Mwenye wetu.

# 7

### *Amuwa tena wafungwa wa shariya*

[1] Niwasowerera wejiwa shariya. Mutikina wanduzangu, kuwa shariya yanawo
uwezo julu ya munu ari hai tu basi? [2] Kwa nfano, mwanamuka wakulombiwa,
alungana naye nlumake nkati ya shariya. Fala ikiwa nlume-yo kafwa, mwanamuka
akuwa na uhuru wa noyi shariya ya ndowa-yi. [3] Ndi ntamana, akilombiwa na nlume
mwengine nlumake ari hai, iye akwitiwa nzinzi. Fala nlumake akifwa, iye akuwa na
uhuru nkati ya shariya, na akilombiwa na nlume mwengine, aawa nzinzi.
[4] Basi, wanduzangu, paufwire mwiri wa Almasihi, nomwe novyo mufwira shariya,
ipate muwe wa mwengine, ire afufuriwe nkifo, muntendere Mwenyezimungu vitendo
vyema. [5] Kamana patikiwa na hali ya kibinadamu, shariya íkisalamula wájibu mbaya
mmwiri mwetu ipate tikore dambi, na mwinsho yawo ndi kifo. [6] Fala sambi tomboriwa
nkati ya shariya konta tifwira cire citifungire, ipate titumike sairi kwa namuna ya mida
ya shariya yandikiwe, ila kwa namuna nyipya ya Roho.

### *Shariya ya Mwenyezimungu ifafanula madambi etu*

[7] Sambi, tikwamba kinani? Shariya ndi dambi? Anta, sivyo-javyo! Kusema kweli,
singari kwijiwa dambi sairi julu ya shariya. Singari kwijiwa kuperereza saisemire
shariya kuwa: “Usiperereze”. [8] Fala dambi ítwala nafasi julu ya ámuri-yo inisalamurira
kila namuna yakuperereza. Kamana, inatowa kuwepo shariya, dambi aingari kuwa
na uwezo. [9] Wakati-wo omi nikiinshingi bila shariya, fala panijiwe ámuri, dambi yanza
kuwepo julu yangu omi, nomi nikifwa. [10] Basi ámuri íkijuzi kuja nawo mainsha kwangu,
falakini inijisira kifo. [11] Kamana dambi itumira nafasi julu ya ámuri-yo initesa, basi
ámuri-yo inulaya. [12] Kwa javyo, shariya kinu takatifu, na ámuri kinu takatifu, kamilifu,
na cema.
[13] Basi, kinu cema cinisalamurira kifo? Kusema kweli, sivyo! Ila dambi itumira kinu
cema kunisalamurira kifo, ipate dambi iwoneke sana-sana kuwa dambi, na julu ya
ámuri izidi kuwa mbaya pakulu.

### *Vita na dambi*

[14] Tikwijiwa kuwa shariya ndi ya Roho, fala omi niwa kibinadamu, epa ni-
uzanyiwa niwa ntwana wa kutumikira dambi. [15] Kamana vyanitenda sereriwa:
vitendo vyanisaka kutenda, sitenda, na vitendo vyakunikima, novyo ndi vyanitenda.
[16] Canitowa kusaka kutenda, nítenda, ntamana omi nikwitikizira kuwa shariya ngema.
[17] Fala sambi, sumi mwanyewe niri kutenda ila dambi iri nkati yangu. [18] Nukwijiwa
kuwa hapana kinu cema cisaka kuwa conse kati ya hali ya kibinadamu. Kweli, nanawo
wájibu wakutenda cema, fala wájibu-wo sitenda. [19] Konta meema anisaka kutenda
sitenda, fala ubaya sanisaka kutenda, nankuzidi kutenda. [20] Basi, omi nikitenda kinu
sanisakula kutenda, mana ake ndi kuwa sumi nitenda, ila dambi iri nkati yangu ndi
itenda.
[21] Kwa javyo, nankuwona kuwa ndi kamba shariya: panisakula kutenda meema,
kitendo kibaya ciwa mbere yangu. [22] Kamana inajibu shariya ya Mwenyezimungu
nkati ya mmoyo mwangu, [23] fala nankuwona uwezo wa shariya nyengine iri nvifingo
vyangu. Ewo uwezo-wo ubishana na shariya ya ankili zangu, initenza kuwa nfungwa
wa uwezo wa dambi iri nvifingo vyangu. [24] Mama! Omi ndi mununi wakuwa na

uzuni-mi! Nani anivusha nkati ya ewu mwiri unipereka kukifo-wu? 25 He! Ninshukuru
Mwenyezimungu kwa sababu ya Insa Almasihi, Mwenye wetu.

Basi nomimi, upande mmoja kwa ankili zangu, nitumika uwezo wa shariya ya Mwenyezimungu. Kwa upande mwengine, kwa mwiri wangu, nitumika uwezo wa dambi.

# 8

*Mainsha a kunfulata Roho wa Mwenyezimungu*

1 Kwa javyo, hapana hukumu ka wanu walungane na Almasihi Insa. 2 Kamana
uwezo wa shariya ya Roho wa mainsha nkati ya Almasihi Insa ukombola nkati ya
uwezo[*] wa dambi na wa kifo. 3 Kinu cakurigariga pakulu upande wa shariya kwa
sababu ya kuveya ka hali ya kibinadamu, kinu-co Mwenyezimungu katenda pam-
pereke Mwanawe mwanyewe, na mwiri wakulandana na wa binadamu wa madambi[†].
Na kuhusu dambi, Mwenyezimungu kahukumu dambi ya binadamu, 4 ipate shuruti
kamili ya shariya itimiziwe kwetu ofwe, ofwe atifulata wájibu mbaya watipongoreriwe
fala tinfulata Roho wa Mwenyezimungu. 5 Kamana ware waínshi na wájibu wa kibi-
nadamu[‡] washugulikira vitendo vya kibinadamu, fala waínshi na Roho washugulikira
vinu vyakumwajibu Roho wa Mwenyezimungu. 6 Namuna zakuwaza za kibinadamu
kifo, ila kunshugulikira Roho Takatifu ndi mainsha na usalama. 7 Kamana namuna
zakuwaza za kibinadamu zibishana na Mwenyezimungu, konta azifulata shariya za
Mwenyezimungu, kusema kweli azikidiri kufulata. 8 Wanu wari nkati ya hali ya
kibinadamu awakidiri kutenda vyakumwajibu Mwenyezimungu.

9 Falakini umwe amuri nkati ya hali ya kibinadamu ila mwankulongoziwa na Roho
wa Mwenyezimungu, ikiwa kweli-kwelini Roho wa Mwenyezimungu muwa naye
mmyoyo mwenu. Mmojawapo ikiwa aana Roho wa Almasihi mmoyo mwake, siyo wake
iye. 10 Ila ikiwa Almasihi kawa mmyoyo mwenu, ingawa mwiri wenu ufwa kwa sababu
ya dambi, fala Roho wa Mwenyezimungu akupani mainsha kwa kuwa mwakikishiwa.
11 Ikiwa Roho wa Mwenyezimungu anfufure Insa ka wafwi kawa mmyoyo mwenu,
noyo akuja kukupani mainsha mwiri wenu wakufwa, julu ya Roho yake iripo mmyoyo
mwenu.

12 Basi, wanduzangu, ofwe tidãiwa, fala sikibinadamu, tisiinshi kibinadamu.
13 Kamana ikiwa muinshi kibinadamu, mwinsho wenu mukufwa. Fala ikiwa mukulaya
vitendo vya kimwiri, julu ya uwezo wa Roho Takatifu, mukuja kuinshi. 14 Kamana piya
walongóziwa na Roho wa Mwenyezimungu, ewo wana wa Mwenyezimungu. 15 Kamana
amupokerere roho yakukutenzani kuwa watwana muludire kutetema kamba mida, ila
mumpokerera Roho Takatifu akutendani kuwa wana wa Mwenyezimungu, ntamana
titamuka kwita "Abba, Baba". 16 Kusema kweli, Roho Takatifu mwanyewe alavya
ushahidi pamoja na roho zetu kuwa tiwa wana wa Mwenyezimungu. 17 Na kwa kuwa
tiwa wanawe, tanawo novyo haki ya kuriti: upande mmoja, tanawo haki kuriti ka
Mwenyezimungu. Upande mwengine, tanawo haki ya kuriti pamoja na Almasihi,
kamana tikitabika naye, tukuja kutukuziwa novyo pamoja naye.

*Tamaa ya furaha ya mbere*

18 Basi sambi, niwalanga kuwa tabu zetu za ewu wakati-wu azijuzi kuringanisiwa na
utukufu usaka kuja watija koloteriwa ofwe. 19 Kamana viyumbe piya wankurindira
na hamu pakulu wakati wawaja kufafanuririwa wana wa Mwenyezimungu. 20 Konta
viyumbe piya vituriwe vyaufwabure, avitenda kinu kwa nafsi yawo ila kwa kusaka ka
ire aturire. Iye katenda javyo kwa tamaa 21 yakuwa viyumbe vikuja komboriwa, visiwe

[*] **8:2** Kigeregu: "uwezo" weta "shariya". [†] **8:3** Ila iye, Insa, aakosa. [‡] **8:5** Wájibu wa kibinadamu ndi wájibu mbaya wapereka munu mwiri wake au kifingo cake kutenda kitendo kimojawapo.

tena vitwana vyakuvunda, viwe na uhuru nkati ya utukufu wa wana wa Mwenyez-
imungu. 22 Kamana tikwijiwa kuwa viyumbe piya viwankurama na viwankutabika
na malwazo a kupongola mpaka sambi-pa. 23 Na sivyo viyumbe basi. Ofwe wanyewe
vyatiwa nawo Roho Takatifu kamba visumo vyakwanza, nofwe novyo wanyewe tanku-
rama patiwarindira na hamu pakulu tilawirire kuwa wanawe, mwiri wetu womboriwe
nfululu. 24 Kamana tivushiwa nkati ya kutumaini tamaa-yo. Ona, kinu cakuwoneka
sico ca tamaa. Kinu ciri kuwoneka, munu awaja na tamaa? 25 Falakini kinu satiwona,
eco ndi catiwa na tamaa, tirindira ka kuvumirira.
26 Sawa-sawa novyo, patisokera Roho Takatifu atisaidiya. Kamana atinéjiwa vyatijuzi
kutenda duwa, fala Roho Takatifu mwanyewe átilebelela ka Mwenyezimungu kwa
namuna saikidirika kwereza. 27 Na ire atúnza ciri nkati ya roho piya§ akwijiwa caawaza
Roho Takatifu, konta iye áwalebelela watakatifu kamba vyaasaka Mwenyezimungu.
28 Ofwe tukwijiwa kuwa, ka wenye kumpenda Mwenyezimungu, piya vinu-vi vikwe-
nendera kuwema ka ware wetiwe watimize mpango wake. 29 Konta wawéjiwe tangu
mwanzo iye kâwatondola wanlande Mwanawe ipate Mwanawe awe ntanzi kati ya
wanduze wengi wawenye. 30 Ware watondoriwe tangu mwanzo, Mwenyezimungu
kaweta. Ware wawetire, iye kawakikisha, na ware wawakíkishe, iye kawawanyira
utukufu wake.

*Hapana cakukidiri kutitanusa nkati ya pendo ra Mwenyezimungu*

31 Kwa javyo, tambani kuhusu vinu-vi? Ikiwa Mwenyezimungu kawa upande wetu,
akidiri kutilumbata nani? 32 Mwenyezimungu aatituwire Mwanawe wawenye, ila
kanlavya kuwa kafara kwa faida yetu ofwe piya. Kwa javyo, namunani vyaatowa
kutipa neye novyo piya vinu?
33 Ware watondoriwe na Mwenyezimungu, ari na haki yakuwawonerera makosa
nani? Mwenyezimungu ndi mwenyé kumwakikisha munu. 34 Mwenyé kuhukumu
nani? Almasihi Insa ndi afwire, visitoshe kafufuriwa ka wafwi, na iye kekala upande
wa nkono nriro wa Mwenyezimungu, novyo iye ndi atilebelela. 35 Atitanusa nani nkati
ya pendo ra Almasihi? Kutabika, tafauti, kulumbatiwa, njala, diki, hatari au upanga?
36 Anta! Kamba vyaandikiwe*:

"Kwa sababu zako uwe, tikulaiwa suku-zi piya,
titafitiwa kamba makondoo vyawokisiwa kusinjiwa."

37 Fala nkati ya piya-vi, ofwe tiwazaidi washindi wakulu, julu ya ire atipendire ofwe.
38 Kamana omi nanawo hakika kuwa wala kifo wala uhai, wala malaika wala wenye
mamulaka, wala mashuguli yetu a rero wala a makeso, wala wenye uwezo, 39 wala
viripo julu au sini, wala kiyumbe cengine kimojawapo, acikidiri kutitanusa nkati ya
pendo ra Mwenyezimungu, rolote julu ya Mwenye wetu, Insa Almasihi.

# 9

*Utungu wa Mwenyezimungu*

1 Kwa kuwa nilungana na Almasihi, nisowera kweli, silongopa. Fahamu yangu julu
ya Roho Takatifu ilavya ushahidi pamoja nomi. 2 Nisowera kweli panisowera kuwa
mmoyo mwangu unijala uzuni nkulu na kulwaziwa sakuna mwinsho. 3 Kamana vinil-
waza mpaka vikinajibu nilaniwe ndaraja ra Almasihi kwa ajili ya wanduzangu, ware
wa kabila yetu moja, 4 niwamba waIziraeli. Ewo waturiwa kuwa wana wa Mwenyez-
imungu, wawona utukufu wake, wapokerera miyadi yakupatana, wagabiziwa Taureti,
wapewa nafasi ya kumwabudu, na wapokerera tamaa zake. 5 Nkati yawo wákiwa

§ **8:27** "Ire atúnza ciri nkati ya roho piya" ndi Mwenyezimungu. * **8:36** Ona Zaburi 44:22.

wababu zawo, na mmoja wawo nkabila yawo ndi Almasihi, Nlungu ari julu ya mambo
piya. Iye Almasihi asifiwe milele! Aamina.
6 Sambi, sikuwa usemi wa Mwenyezimungu ukosa. Kamana sikuwa piya ware wa
Iziraeli kibinadamu, waIziraeli wakweli, 7 wala sikuwa piya wa rikolo ra Iburahima
ujukulu wake. Konta Mandiko akwamba: "Wajukuluwo zina rawo ndi riwalangiwa
julu ya Izaki." 8 Kinu-ci mana ake ndi kuwa wana wapongoriwe kibinadamu siwo
wana wa Mwenyezimungu ila wana wapongoriwe kamba vyaalavire tamaa ndi
wawalangiwa kuwa ujukulu. 9 Konta tamaa isema javi:
"Kwa muda wa mwaka mmoja nukuja,
na Sara ampongola mwana mmoja nlume."
10 Visitoshe, Rebeka cinkuna kinu kimoja paawemite wanawe na nlume mmoja,
Izaki baba wetu. 11 Anta wanawe sawanapongoriwa, wala sawanatenda cema wala
kibaya, Mwenyezimungu kantondola mwana mmoja ipate vyaalangele Mwenyez-
imungu kuhusu kutondola kwake kwendeleye, siyo kwa vitendo fala awepo wakwita,
12 iye kambiriwa javi: "Mwana ntanzi akuja kuntumika wa mwinsho." 13 Kamba
vyavyandikiwe mMandiko: "Yankubu nimpenda, Ezau nimwina*."
14 Sambi tambe mwaja? Mwenyezimungu aana shariya? Anta siyo javyo! 15 Kamana
kamwambira Musa javi†:
"Nintendera huruma waninsaka onse,
nimmonera utungu anajibu onse."
16 Kwa javyo, avikuna kamba vyatisaka au vyatitenda ila vikuna kwa uwezo wa
mwenyé kutendera huruma, Mwenyezimungu tu basi. 17 Javi ndi vyaasowere
Mwenyezimungu mMandiko Matakatifu, akimwambira nfalume wa Miswiri:
"Ndi noco canukuturire kuwa nfalume ipate julu ya uwe nolote uwezo wangu,
na zina rangu rijiwikane ulumwengu nzima-wu piya."
18 Kwa javyo, iye antendera huruma waansaka, na antula kuwa ngumu waansaka.
19 Umwe nanga munidairi javi: "Sababuni iye kuwapa wanu ukosa? Kamana akidíri
kubishana na vyaasaka iye nani?" 20 Fala uwe binadamu, kuwa nani wakunsutumu
Mwenyezimungu? Kiyungu cakufiyangiwa cindairi afiyange kwamba: "Sababuni
kunifiyanga javi?" 21 Munu wakufiyanga, akitwala utope akifiyanga nringi wapambari,
na utope mmoja nowo akifiyanga nringi mwengine wakutumiriwa pakaya, aana
mamulaka a kutenda javyo? 22 Sikuwa Mwenyezimungu ásaka kolota kukimiwa kwake
na kwijiwisa uwezo wake? Ntamana iye ketamili na imani pakulu miringi yejaze
nyongo yake, yaatengeze kwaribiwa, 23 ipate ejiwise novyo utajiri wa utukufu wake ka
miringi yejaze huruma zake, yaatengeze mida kupokerera utukufu wake. 24 Miringi-yo
ndufwe titondoriwe na Mwenyezimungu. Atitondoriwe nkati ya Mayahudi tu basi, fala
nkati ya Sawari-Mayahudi newo novyo. 25 Kamba Mwenyezimungu vyaambire julu ya
nabii Ozeya‡, akamba javi:
"Niweta wanu sawari wangu, wawe wanu wangu;
niweta sawari wapendani wangu, wawe wapendani wangu."
26 Novyo:
"Na vikuja kukuna mahala pawâmbiriwe javi: 'Umwe amuri umati wangu',
mahala-po ewo wakuja kwitiwa 'wana wa Mwenyezimungu hai.' "
27 Izaya nneye kankukuwa kuhusu Iziraeli, akwamba§:
"Ingawa ujukulu wa Iziraeli mwingi
kamba misanga ya mwani,
fala aba javi ndi waja kuvushiwa."

* **9:13** "Nimwina" epa mana ake "omi ninkatala". † **9:15** Ona Kulawa 33:19. ‡ **9:25** Ona Ozeya 1:10. § **9:27** Ona Izaya 10:22-23.

28 Konta kulamula kwake muardhi, Mola aakawisa na atimiza nfululu. 29 Kamba tangu
mida vyaâsemire Izaya, akamba:
"Inawa Mola, Mwenyé Uwezo, aâtasire ujukulu* anta aba,
nanga tiwa kamba Sodoma,
nanga tilanda Gomora."

*Iziraeli na Habari Ngema*

30 Sambi, kuhusu novi vinu-vi, tikwamba kinani? Tikwamba kuwa Sawari-Mayahudi
awakisakula ukamilifu, wakipata, fala vikuna julu ya kuntumaini Mwenyezimungu.
31 Upande mwengine, Mayahudi wakisakula ukamilifu julu ya kufulata shariya, fala
awapatire. 32 Konta ya kinani? Konta namuna zawo azíkiwa julu ya kwamini ila zíkiwa
julu ya vitendo vyawo. Wakwakula riwe rakukwakuriwa, 33 kamba vyayandikiwe†:
"Ona, nankutula Ziyoni‡ riwe rawaja kukwakula,
riwe risaka kuwagwisa.§
Mwenyé kuntumaini iye, aaja kuriwonera haya."

# 10

1 Wanduzangu, vinajibu pakulu mmoyo mwangu na niwanlebelela ka Mwenyez-
imungu Mayahudi wavushiwe. 2 Omi niwa shahidi kuhusu ewo kuwa wanawo hamu
pakulu na Mwenyezimungu, fala noyo hamu-yo airi nkati ya kumwijiwa. 3 Kamana
awejiwa ukamilifu ulawa ka Mwenyezimungu, ila wasakula kubainisha ukamilifu
wawo wanyewe. Kwa javyo, awasaka kupokerera ukamilifu wakulawa ka Mwenyez-
imungu. 4 Kamana Almasihi ndi kusudi ya shariya, impa ukamilifu kila mwenyé
kumwamini.

*Wanu piya wanawo nafasi ya kuvushiwa*

5 Musa kandika kuhusu ukamilifu ulawa julu ya kufulata shariya. Kaamba javi:
"Mwenyé kufulata ámuri za shariya, áinshi julu yake." 6 Fala ukamilifu julu ya
kumwamini Mwenyezimungu ukwamba: "Usambe mmoyo mwako: 'Asáka kukwera
mbinguni nani?' " Kwamba javyo, Almasihi umwisusa. 7 "Wala: 'Asáka kwisukira
mahala ka wafwi nani?' " Konta eco Almasihi kunlamusa ka wafwi. 8 Musa kankwamba
kinani? Iye akwamba javi:
"Usemi uwa karibu yako,
nkanywa mwako na mmoyo mwako."
(Mana ake ndi usemi watitangaza, kuwa tijuzi timwamini Mwenyezimungu.) 9 Kamana
ukisowera na kanywa yako kuwa Insa ndi Mwenye, na ukamini mmoyo mwako
kuwa Mwenyezimungu kanfufula nkifo, ukuja kuvushiwa. 10 Kamana mmoyo munu
akamini, apata kwakikishiwa. Julu ya kusema na kanywa yake, apata kuvushiwa.
11 Konta Mandiko akwamba javi:
"Munu asáka kuwa onse akimwamini Mwenyezimungu, aimpata aibu."
12 Akupo kusiyana nkati ya Mayahudi na Sawari-Mayahudi. Mwenye mmoja ndi
Mwenye wa wanu piya, na iye ndi mwenyé utajiri ka piya wenye kunlebela. 13 Kamana
"Munu asaka kuwa onse anlébela Mwenye akuja kuvushiwa."
14 Fala wanu wanlebelaja sawanamba kumwamini? Na wamwaminija sawanasikira
akitamburiwa? Na wasikiraja sawerepo munu wakuwereza Habari Ngema? 15 Na
wanu wokaja kwereza sawaperekiwe? Kamba vyandikiwe Mandiko Matakatifu:
"Namuna vyasitawire maulu a ware wapita wakereza Habari Ngema."
16 Fala siyo kuwa Mayahudi piya wafulata Habari Ngema. Kamana Izaya kasema javi:
"Mola, amíni habari zetu nani?"

* **9:29** Kigeregu: "mbeyu". † **9:33** Ona Izaya 8:14; 28:16. ‡ **9:33** "Ziyoni" mana ake "Yerusalemu". § **9:33** "Riwe risaka kugwawisa" mana ake Mwenye Insa.

17 Basi, kwamini kukuja na kusikira Habari Ngema, na kusikira Habari-yo ikuja nkati
ya kwereza kuhusu Almasihi.
18 Fala nukwamba, Mayahudi piya awasikire? Kusema kweli, wasikira. Mandiko
awenye akwamba*:
"Shauti zawo zenera ardhi piya,
usemi wawo ufika mpaka mwinsho wa ulumwengu."
19 Nukwamba, itakuwa wanu wa Iziraeli awereriwe? Aye, wereriwa. Cakwanza, julu
ya Musa†, Mwenyezimungu kaamba javi:
"Omi nukushongani muwatendere wiyana wanu sawari wa taifa.
Julu ya taifa watikinifu, nukukimwisani."
20 Julu ya Izaya‡, Mwenyezimungu karikomarisa, kaamba javi:
"Nisinganiriwa na wanu sawakinisakula,
nirolota ka wanu sawakinidairi."
21 Fala ka Iziraeli, Mwenyezimungu kaamba javi:
"Suku daima-zi nikolosa makono angu kwawo ewo,
fala ewo awanisikiriza, wanikaidi."

# 11

*Mwenyezimungu awakatala waIziraeli piya*

1 Sambi, omi nídairi: Mwenyezimungu wanu wake kawakatala? Anta! Omi
mwanyewe niwa muIziraeli, ujukulu wa Iburahima, na wa rikolo ra Benjami.
2 Mwenyezimungu aawakatare wanu wake wawatondore tangu mwanzo.
Au amukumbukira vyaamba Mandiko Matakatifu kuhusu Aliyasi, namuna
vyanlalamikira Mwenyezimungu kuhusu wanu wa Iziraeli? 3 Iye kaamba javi:
"Mola, ewo minabii wako wawolaya,
mauralu ako a kafara wadangula.
Ila wanasa omi tu basi yeka yangu,
na wanisakula nomi novyo wanulaye."
4 Mukumbukira majibu a Mwenyezimungu mbere yake? Akwamba:
"Niriturira omi mwanyewe wanu alufu saba sawankokorere Baal!"
5 Na wakati wa rero-wu ndi novyo, ribaki kundi ra wanu aba futi, watondoriwe kwa
rehema ya Mwenyezimungu. 6 Kutondoriwa-ko kuwa julu ya rehema, aiwere kwa
sababu ya vitendo vyawo wanu-wo. Kamana rehema yakupatikana julu ya vitendo siyo
rehema.
7 Sambi tambe, mwaja? Cawakisakula Mayahudi, kinu-co awapatire. Ila wanu
watondoriwe ndi wapatire. Wengine-wo wataiwa myoyo migumu. 8 Kamba vyaamba
Mandiko*:
"Mwenyezimungu kawapa roho ya usingizi,
maso sawona, na masikiro sasikira,
mpaka rero-vi."
9 Daudi neye novyo kasema javi†:
"Sherehe ya vyakurya vyawo iwe nambo na kiruzi,
cakuwakwakurisa awe ndi maripo awo.
10 Kuwenukare kumaso wasiwone,
iwatumbe miyongo yawo suku piya-zi."

*Kuvushiwa ka wanu Sawari-Mayahudi*

11 Kwa javyo, nídairi tena: Mayahudi wakwakula, wagwe milele? Sivyo javyo! Ila
kwa kuwa ewo wakosa, kuvushiwa kuja kwa ajili ya wanu Sawari-Mayahudi, kuwataye

* **10:18** Ona Zaburi 19:4. † **10:19** Ona Kumbukumbu 32:21. ‡ **10:20** Ona Izaya 65:1. * **11:8** Ona Kumbukumbu 29:4. † **11:9** Ona Zaburi 69:22-23.

wivu Mayahudi. 12 Basi, ikiwa ukosa wawo uwatenza wanu mulumwengu-mu kupata
utajiri, na kupunguka kwawo ndi utajiri wa Sawari-Mayahudi, utajiri nkulu pakulu
ulawirira Mayahudi pawasaka kuludira ka Mwenyezimungu!
13 Epa nankukwambirani umwe, Samuri-Mayahudi. Kwa kuwa omi niwa walii wa
wanu Sawari-Mayahudi, nintukuza Mwenyezimungu kwa kazi yanipere. 14 Konta,
kwa namuna mojawapo, nisaka niwashonge wanu wa kabila yangu wawe na wivu,
niwavushe wamojawapo. 15 Kamana, ikiwa kutuwisiwa kwawo ndi sababu ya
wanu wa mulumwengu-mu kupatana na Mwenyezimungu, vikuja kukuna mwaja
wakikubaliwa? Ndi kamba kuludisiriwa uhai bandi ya kufwa, sinovyo? 16 Ikiwa mikate
yakwanza kociwa takatifu, na ibakire neyo takatifu. Na ikiwa nzipe wa muti takatifu,
na vitambi nevyo takatifu.‡
17 Ikiwa visinjiwa vitambi vimojawapo vya muti§, na uwe kitambi ca nzaituni wa
nnundu cikilunganisiwa nawo, cisanganyika na mizipe ya nzaituni mwema, cipata
unoni wake*, 18 basi usiridãi julu ya vitambi visinjiwe vire. Ukiridãi, kumbukira
kuwa uwe siwitamili nzipe-wo, ila nzipe-wo ndi ukwitamili uwe. 19 Dalili ukwamba:
"Visinjiwa vitambi ipate nilunganisiwe omi." 20 Vyema, ila kumbukira kuwa vitambi-
vyo visinjiwa kwa sababu yakutowa kumwamini Mwenyezimungu. Na uwe koloka
kwa sababu ya kwamini. Usiwaze kuridãi, ila wopesiwe. 21 Kamana Mwenyezimungu,
ikiwa aasire vitambi kaanuni, futi uwe, aatakukwasa.
22 Kwa javyo, tunza wema na ukali wa Mwenyezimungu: upande mmoja, iye nkali
ka ware wagwire, upande mwengine, iye akutenda meema, ukizidi kuinshi nkati
ya wema wake. Ukasa, nnowe novyo ukuja kusinjiwa. 23 Mayahudi novyo, wak-
iludira kumwamini Mwenyezimungu, ewo walunganisiwa. Kamana Mwenyezimungu
kanawo uwezo wakuwaludisira kuwalunganisa. 24 Kamana uwe ndi kamba kita-
mbi cakusinjiwa munzaituni kaanuni wa nnundu, cilunganisiwe munzaituni waku-
vyariwa ingawa sico kaanuni. Futi vitambi kaanuni vilunganisiwe munzaituni wawo
wawenye?

### *Huruma ya Mwenyezimungu ka wanu piya*

25 Wanduzangu, vinajibu musitikine eyi siiri ya kweli-yi ipate musiwaze kuwa
mwa wejiwifu pakulu. Eyi siiri-yi ndi kuwa Mayahudi wamojawapo myoyo yawo
ilawirira kuwa migumu mpaka isabu ya wanu Sawari-Mayahudi Mwenyezimungu
waapangire kuvushiwa, wavushiwe. 26 Kwa javyo, piya Iziraeli ikuja kuvushiwa,
kamba vyavyandikiwe†:
"Nvushi akuja kulawa Ziyoni‡,
akuja kulavya ubaya wa waIziraeli§.
27 Na eyi ndi miyadi yaniwaturire ewo,
panija kuwalavya madambi awo."
28 Upande mmoja, kuhusu Habari Ngema, ewo maaduwi wa Mwenyezimungu kwa
faida yenu. Fala, kwa kuwa Mwenyezimungu kawatondola, ewo wapendiwa pakulu
kwa sababu ya tamaa yawâpewe wababu zawo. 29 Kamana Mwenyezimungu aapindula
mawazo ake kuhusu wanu wawatondola na uwezo maalumu awajanliya. 30 Mida
umwe amukinsikirizanga Mwenyezimungu, fala sambi-pa moloteriwa huruma kwa
sababu ya ubishi wawo. 31 Kwa namuna moja novyo, Mayahudi sambi-pa awansikiriza
Mwenyezimungu ipate kwa sababu ya huruma yamoloteriwe, newo novyo sambi-pa

‡ **11:16** Mana ake: Kwa kuwa Iburahima pamoja na wababu zetu wengine wákiwa wanu wa Mwenyezimungu, wana wawo newo novyo wakuja kuwa wa Mwenyezimungu. § **11:17** Mana ake: Mayahudi wamojawapo wakilaviwa. * **11:17** Mana ake: umwe mukuja kupokerera baraka zaalavire tamaa Mwenyezimungu akinlaizira Iburahima pamoja na wanawe. † **11:26** Ona Izaya 27:9; 59:20-21. ‡ **11:26** "Ziyoni" mana ake "Yerusalemu". § **11:26** Kigeregu: "Yankubu".

woloteriwe huruma. 32 Basi, kwa sababu ya ubishi wa wanu piya, Mwenyezimungu
awatula kamba wafungwa ipate awolotere wanu piya huruma yake.
33 He, namuna vyauri nkulu utajiri wa Mwenyezimungu! Na vyaziri nyingi fahamu
zake na wijiwifu wake! Nani afafánula vyaalamula iye? Nani erériwa mipango yake?
34 Kamba vyaasema Mandiko*:
"Nani ejíwa ankili za Mola?
Nani akidiri kunlanga iye?
35 Mununi ampere kinu Mwenyezimungu
kwa kuwa ajuzi kuripiwa?"
36 Konta piya vílawa kwake iye, julu yake iye, na kwa faida yake iye. Mwenyezimungu
apewe utukufu wa milele! Aamina.

# 12

*Mainsha a kuntumika Mwenyezimungu*

1 Kwa javyo, wanduzangu, kwa sababu ya huruma ya Mwenyezimungu,
nukutafadalini mwiri wenu-wo mupereke nfululu ka Mwenyezimungu, uwe kafara
hai na takatifu, kamba vyavimwajibu iye. Eyi ndi ibada yako ya kweli. 2 Musiinshi
vyawainshi wanu wa mulumwengu-mu, ila mwaseni Mwenyezimungu akupindureni
ankili zenu muwe na mawazo mapya. Tendani javyo ipate mwijiwe vyaasaka
Mwenyezimungu, vyema, vyakwajibisa, na vyakukamilika.
3 Kamana, kwa sababu ya rehema yanipewe, nukulaizirani umwe kila mmoja:
musiriwone pakulu kupunda camuri-co. Ila kila mmoja awaze kunyenyekeya
mwanyewe kwa namuna ya kwamini Mwenyezimungu vyaantongera kila mmoja.
4 Kamana kamba mwiri mmoja vyauri nawo vifingo vingi, fala vifingo-vyo piya avi-
tenda kazi moja, 5 ndi sawa-sawa nofwe: tiwa wengi, fala kwa kuwa tilungana na
Almasihi, tiwa mwiri mmoja, na kila mmoja kifingo ka mwenziwe. 6 Mwenyezimungu,
julu ya rehema yake, katipa neema ya uwezo jisijisi. Apéwe uwezo wakubushuru,
atende kwa kufulata kiyasi ca kwamini kwake. 7 Apéwe uwezo wakutumika, atumike.
Ikiwa wakufunda, afunde. 8 Apéwe uwezo wakuwarimbisa myoyo wenziwe, basi
awarimbise myoyo. Apéwe uwezo wakumera, amere asiwe na coyo. Apéwe uwezo
wakuwalongoza wenziwe, awalongoze kwa juhudi. Apéwe uwezo wakuwolotera wanu
huruma, atende kwa radi.

*Shuruti za wenye kwamini*

9 Kupenda kwenu kuwe ka kweli. Ubaya ukukimeni, rimbisani kutenda meema.
10 Pendanani munu na mwenziwe kwa pendo ra unduyu, na mwinshimiyane kwa
juhudi. 11 Tenderani juhudi kazi, musiwe wafuko. Ntumikeni Mwenye kwa roho ya
kukulunguzani. 12 Nkati ya tamaa, furahini. Nkati ya tabu, vumirirani. Na nkati ya
duwa, zidini kulebela. 13 Wasaidiyeni wenye kwamini. Na wayeni wapokerereni na
jitiyadi.
14 Wanu wakulumbatani, nlebeleni Mwenyezimungu awabariki. Lebelani wajanli-
iwe, musiwalani. 15 Wenzenu wari kufurahi, furahini nawo. Wenzenu wari kurira,
rirani nawo. 16 Munu na mwenziwe, mutafitiyane kwa namuna moja noyo. Musiri-
ture ubora, ila pamulongoziwa murinyenyekeye. Musiriwone kuwa wejiwifu umwe
wanyewe!
17 Musiripirirane na munu awa onse, ubaya ka ubaya. Tendani wanu vyawawona
piya kuwa vyema. 18 Camukidiri umwe wanyewe, tenderani juhudi muinshi salama
na wanu piya. 19 Wapendani wangu, musishupane watupu ila mwasireni nyongo
Mwenyezimungu atende shariya.

* **11:34** Ona Izaya 40:13.

Konta yandikiwa javi*:
"Omi ndi mwenyé maripo a ubaya.
Omi ndi nija kuripa, amba ndi Mola."
20 Fala,
"Aduwi wako, ikinkola njala, mpe cakurya.
Ikinkola nyotwa, mpe maji.
Ukintenda javyo,
aduwi wako kuntula makala a moto patumela,
alama ya kuntenza aya."†
21 Usishindiwe na ubaya, ila shinda ubaya na meema.

# 13

### *Kusikiriza mamulaka*

1 Kila munu ariture kusikiriza mamulaka a mafalume, konta aangari kuwepo ma-
mulaka a ufalume bila Mwenyezimungu. Piya wenye mamulaka, iye ndi awaturire.
2 Basi, wanu wakukatala mamulaka a ufalume wawankubishana na kauli ya Mwenyez-
imungu. Na ware wabishana naye, wakuja kuhukumiwa. 3 Kusema kweli, mafalume
awawataya wofi waténda meema, ila wawataya wofi, waténda ubaya. Úkisaka usiwope
wenye mamulaka? Basi, tenda meema, ukuja kusifiwa nawo. 4 Kamana mwenyé
mamulaka antumikira Mwenyezimungu kwa wema wako uwe. Fala, ukitenda ubaya,
ukuwa mofi, konta iye aakusukurira bakora* bure-bureni. Kamana iye ndi ntumisi
wa Mwenyezimungu wakunshupa na wakunlavira nyongo aténda ubaya. 5 Ntamana,
ibidi kuwasikiriza wenye mamulaka, siyo kwa kunyema nyongo ya Mwenyezimungu
tu basi, fala novyo ipate fahamu zako zitengemane.

6 Kwa namuna moja novyo waripeni nsoko, konta ewo watumisi wa Mwenyez-
imungu, washugulikira kazi-yo suku daima. 7 Nripeni kila mmoja camujuzi kunripa:
nripeni nsoko munu wamujuzi kunripa nsoko, mpeni ncango munu wamujuzi kumpa
ncango, mopeni wamujuzi kumopa, na nsifuni ire wamujuzi kunsifu.

### *Kutimiza shariya julu ya kuwapenda wenzenu*

8 Musiwiriwe anta kinu, sairi kupendana, konta ampénda munu mwengine, atimiza
piya ámuri ziri nkati ya shariya. 9 Kamana ámuri-zo zikwamba, "Usizinge", "Usiulaye",
"Usiwe", "Usiperereze", na ámuri vyaziri piya, zijumulanisiwa kwa ámuri mmoja tu
basi: "Mpende mwenziwo kamba vyauripenda uwe mwanyewe." 10 Munu ampénda
mwenziwe aantenda ubaya. Kwa javyo, kuwa na pendo ndi kutimiza shariya.

11 Visitoshe, mukijiwa enzi zatiri-zi, kuwa ufika futi wakati wakusisimuka. Ka-
mana epa sambi kuvuka kwetu kuwa karibu pakulu koliko patanzire kunkubali Insa.
12 Usiku wankupita, kuca kuwa karibu. Basi, tase vitendo vya kisi, ila tivare sulaha
za panlangaza. 13 Tiinshi kwa namuna ngema kamba wanu wari kuinshi nsana juwa
rikiwala. Musipite mmajambo a kurewiwa pakulu, wala musirewe. Musizinge, wala
musitende kitendo kimojawapo ca ceje. Musumane, wala musiwatendere wiyana wen-
zenu. 14 Kwasa evyo, rikengereni na kuwapo ka Mwenye Insa Almasihi. Musisakure
kurinafusi wájibu wenu mbaya wa kibinadamu.

# 14

### *Musiwalaumu wenzenu*

1 Sawana nguvu nkati ya kwamini, wapokerereni, wala musiwakaidi mawazo awo.
2 Munu mmojawapo akwamini kuwa kanawo haki ya kurya kila namuna ya cakurya,

* **12:19** Ona Kumbukumbu 32:35. † **12:20** Ona Usowezi 25:21-22. * **13:4** Kigeregu: "upanga, alama ya kuulaya".

fala wakwamíni aba akurya unde na masamba tu basi. 3 Munu árya cakurya kimo-
jawapo asikejeli cakurya saarya. Na saarya cakurya kimojawapo, asinlaumu munu
wakurya piya vinu, konta Mwenyezimungu kawapokerera nowo wanu-wo. 4 Uwe
nani wakusaka kunlaumu ntumisi wa munu mwengine? Ntumisi-yo akuja koloka
au kwinama mbere ya mwenye wake. Kweli, iye akuja koloka konta Mwenye Insa
akidiri kumolosa. 5 Munu mmojawapo awaza kuwa iwapo suku bora pakulu koliko
suku nyengine, fala munu mwengine atula kuwa suku piya sawa-sawa. Sikirizani,
kila munu oloke na mawoni ake. 6 Atúla kuwa iwapo suku maalumu atenda novyo
ansifu Mwenye. Na árya vyakurya piya, akurya ka kunsifu Mwenye, konta anshukuru
Mwenyezimungu. Na sawarya, newo novyo watenda javyo ajili ya kunsifu Mwenye, na
wanshukuru Mwenyezimungu. 7 Kamana kati yetu aapo munu ainshi kwa nafsi yake
mwanyewe, wala aapo afwa kwa nafsi yake mwanyewe. 8 Ikiwa tankuinshi, tiinshi
kunsifu Mwenye. Ikiwa tukufwa, tukufwa kunsifu Mwenye. Kwa javyo, anta tiinshi
au tifwe, tiwa wa Mwenye. 9 Kamana kwa sababu ya noco, Almasihi kâfwa na kaludira
kuinshi, ipate awe Mwenye wa wafwi na wari hai.
10 Sambi, uwe, konta ya kinani kunlaumu nduyo? Na uwe, sababuni kunkejeli nduyo?
Kamana ofwe piya tukuja kujibu mbere ya Mwenyezimungu tilamuriwe. 11 Konta
vyandikiwa*:

“Kamba kweli-kwelini niwapo, amba ndi Mola,
